


MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI



24/05/2022

TANGAZO LA MNADA WA KEMIKALI

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) itauza kwa njia ya Mnada wa hadhara jumla ya kemikali 363 tarehe 06/06/2022 kuanzia saa nne 4.00 asubuhi kwenye Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Ziwa Mwanza iliyoko Isamilo jirani na hospitali ya Sekou Toure.

MASHARTI YA MNADA

1. Wadau wa kemikali waliosajiliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tu ndiyo watakaoruhusiwa kushiriki na kununua kemikali katika mnada.
2. Kila mdau wa kemikali atakayehudhuria mnada huu atatakiwa kuonesha cheti cha usajili "**Certificate of Registration**" kinachotolewa na Ofisi ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali kabla ya kuruhusiwa kushiriki mnada huo.
3. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia **Mia Moja (100%)** ya thamani ya kemikali atakayonunua, na kukamilisha malipo yote. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kemikali na amana iliyolipwa **haitarudishwa**.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua kemikali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia/ kukagua kemikali itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya kufanyika mnada husika kwa saa za kazi.
6. Mnada utaanza saa Nne (04.00) asubuhi katika ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kanda ya Kanda ya Ziwa Mwanza iliyoko Isamilo jirani na hospitali ya Sekou Toure.

Imetolewa na;

Sylvester Omary

**Msimamizi wa Kitengo Cha mawasiliano na Uhusiano
kwa Umma.**

S/N	MAELEZO	KIPIMO	IDADI
1	Ultrawhite Hydrated Lime	Mifuko/25kg	200
2	Activated Carbon	Mifuko/25kg	20
3	Sodium Cyanide	Drum/50kg	15
4	Gololi za crusher	Mifuko/48pcs	10
5	Katani	Barlow	1
6	Empty Drums	Pc	117
7	Ethanol	Drum/0.5	1